Jumapili ya 25 - Mwaka C

# EE BWANA MBELE YA MIUNGU

**Zab. 138:1-5, 7-8 (K) 1**

M.B. Chuwa
Moshi




1. (a) Nitakushukuru kwa moyo wangu wote, mbele ya Miungu nitakuimbia zaburi
   (b) Nitasujudu nikilikabili hekalu lako takatifu, nitalishukuru jina lako.

2. (a) Nitalishukuru jina lako, kwa ajili ya fadhili zako na uaminifu wako, kwa maana umeikuza ahadi yako kuliko jina lako,
   (b) Siku ile niliyokuita uliniitikia, ukanifariji nafsi kwa kunitia nguvu.

3. (a) Ee Bwana wafalme wote wa dunia watakushukuru, watakapoyasikia maneno ya kinywa chako,
   (b) Naam wataziimba njia za Bwana, kwa maana utukufu wa Bwana ni mkuu.

4. (a) Utanyosha mkono juu ya hasira ya adui zangu, na mkono wako wa kuume utaniokoa;
   (b) Bwana atanitimilizia mambo yangu. Ee Bwana fadhili zako ni za milele, usiziache kazi za mikono yako.